SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jarida la

# RELI NA MATUKIO

Toleo namba 21, Juni 2022

Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

## RAIS SAMIA APOKEA TUZO YA MJENZI BORA AFRIKA 2022




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akipokea Tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022 kutoka kwa Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Solomon Quaynor kwa niaba ya Rais wa Benki hiyo Dkt. Akinumwi Adesina, Accra nchini Ghana Mei, 2022.

Na Mwandhishi wetu

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan amepokea tuzo ya Babacar Ndiaye (2022) kwa mafanikio ya Serikali ya awamu ya Sita katika ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji, katika Mkutano wa 57 wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) nchini Ghana, Mei 2022.

Tuzo hiyo hupewa viongozi wa Afrika walio mstari wa mbele katika kuendeleza miundombinu. Katika hafla hiyo, Rais Samia ametoa wito kwa nchi za Afrika kuungana, kuzijenga na kuziwezesha jumuiya za kiuchumi za kikanda na bara kwa ujumla.

Rais Samia amesema lengo la ujenzi wa miundombinu Tanzania ni kuunganisha nchi, ukanda wa Afrika Mashariki na nchi za SADC ili kufikia agenda ya utangamano wa Afrika kiuchumi na kijamii.

Inaendelea Uk. 2

## KATIBU MKUU KIONGOZI AKAGUA BANDARI KAVU NA KARAKANA YA SGR Uk. 3



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa akimuelezea Katibu Mkuu Kiongozi kuhusu namna karakana na kituo cha treni za kisasa za mizigo Kwala kitakavyofanya kazi pamoja na bandari kavu ya Kwala mkoani Pwani Mei, 2022.

# RAIS SAMIA APOKEA TUZO YA MJENZI BORA AFRIKA 2022

Inatoka Uk. 1

Rais Samia amesema ni lazima Afrika izalishe, ichakate na ifanye biashara ndani ya bara ili Soko Huru la Bara la Afrika (AfCFTA) liweze kutimiza malengo.

Vile vile, Rais Samia ameongeza kuwa maendeleo ya miundombinu ni mchakato endelevu, hivyo anatambua michango ya Marais waliotangulia katika ujenzi wa miundombinu ya uchukuzi nchini kupitia Mfuko wa Barabara na Taasisi za kifedha za kimataifa.

"Nikitambua napokea tuzo hii nikiwa bado siamini kwamba tuzo hii inaweza kuwa ya mtu binafsi, mimi naamini tuzo hii inatakiwa iwe ya mtu mmoja anayestahili kuliko wote Tanania ni Dkt. John Pombe Magufuli" amesema Rais Samia

Rais Samia amesema kuwa jitihada za ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji zilianzishwa katika awamu tano za uongozi zilizopita lakini katika jitihada hizo hayati Magufuli alijitokeza zaidi kwa kuwa alikuwa Waziri wa Ujenzi katika Serikali ya awamu ya tatu chini ya Hayati Benjamin Mkapa na awamu ya nne chini ya Jakaya Kikwete

Rais Samia amewashauri wakuu wa nchi kuweka mikakati madhubuti ya usimamizi wa rasilimali za bara la Afrika ikiwa ni pamoja na kuimarisha ukanda wa biashara ili zinufaishe wananchi. Ili kufanikisha hilo Rais Samia ameshauri nchi za Afrika kuimarisha miundombinu ya usafirishaji hasa barabara na reli kwani ni kigezo muhimu katika kuunganisha bara hilo na fursa za kiuchumi.

Serikali ya Tanzania inatekeleza miradi ya kuimarisha miundombinu ya barabara na reli ambapo kwa kipindi cha awamu ya sita chini ya Rais Samia, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa reli ya kisasa – SGR Dar es Salaam hadi Makutupora mkoani Singida pamoja na kuanza kipande cha Makutupora – Tabora na Mwanza – Isaka. Pia Serikali ipo katika hatua za mwisho za mchakato wa kuanza utekelezaji wa kipande cha Tabora – Isaka kilichosalia ili kukamilisha awamu ya kwanza ya mradi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza.

Aidha, Rais Samia ameishukuru Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) kwa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Tanzania katika kuboresha miundombinu nchini akisisitiza kuwa anajisikia mwenye faraja kubwa kwa kufanikiwa kukamilisha baadhi ya miradi mikubwa ya miundombinu ndani ya muda mfupi wa uongozi wake.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan, akionesha Tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022 (Babacar Ndiaye Trophy 2022), mara baada ya kukabidhiwa Tuzo hiyo na Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda katika Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Solomon Quaynor Accra nchini Ghana, Mei 2022.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan (kati), akiwa katika picha ya pamoja na Makamu wa Rais wa Sekta Binafsi, Miundombinu na Viwanda katika Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) Solomon Quaynor pamoja na viongozi mbalimbali wa Benki hiyo mara baada ya kukabidhiwa Tuzo ya Babacar Ndiaye kwa mwaka 2022.

# KATIBU MKUU KIONGOZI AKAGUA BANDARI KAVU NA KARAKANA YA SGR

Inatoka Uk. 1



Mkurugenzi Mkuu TRC Masanja Kadogosa akielezea mikakati ya Shirika katika kuongeza ufanisi wa usafirishaji mizigo wakati wa ziara ya Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Hussein Kattanga katika bandari kavu ya Kwala mkoani Pwani Mei, 2022.

Katibu Mkuu Kiongozi Balozi Hussein Kattanga amekagua bandari kavu ya kwala pamoja na kituo cha treni za kisasa za mizigo na karakana, Kwala mkoani Pwani Mei, 2022.

Katibu Mkuu Kiongozi ameeleza kuwa lengo la ziara hiyo ni kuzikutanisha Wizara na taasisi zinazohusika na mradi wa bandari kavu ya Kwala, kuweka mawazo ya pamoja, kuzungumza na kukubaliana kufanya kazi ili eneo la bandari kavu ya Kwala lianze kufanya kazi.

Balozi Kattanga amefanya ziara hiyo akiambatana na Makatibu wakuu wa wizara mbalimbali ikiwemo Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Uwezeshaji, TAMISEMI pamoja na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Viongozi wengine waliohudhuria ni pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania, Mamlaka ya Bandari Tanzania, DAWASA, Shirika la Umeme Nchini, Mkuu wa mkoa wa Pwani Katibu Tawala mkoa wa Pwani pamoja na Mkurugenzi wa Wilaya ya Kibaha.

Aidha, Katibu Mkuu Kiongozi amewasisitiza wakuu wa taasisi na viongozi kila mmoja katika nafasi yake kufanya jitihada za kuhakikisha eneo la Kwala linaanza kufanya kazi kwa kutimiza wajibu wa kufikisha huduma muhimu katika eneo hilo la kimkakati

“Nikirudi tena nataka nione biashara zinaendelea, ninakwenda kutoa ripoti kwa Mhe. Rais kuwa wafanyakazi wako tayari kuhakikisha kazi zinaenda na zitaenda” alisema Balozi Kattanga

Kwa upande wa Shirika la Reli Tanzania – TRC kupitia taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika Ndugu Masanja Kadogosa amesema kuwa Shirika la Reli tayari limekamilisha ujenzi miundombinu ya reli ya MGR katika eneo la bandari na eneo la Karakana na kituo cha treni za mizigo za reli ya kisasa - SGR.

Halikadhalika uongozi wa Mkoa wa Pwani umesema kuwa umejipanga kuhakikisha maeneo yaliyopo karibu na bandari kavu ya Kwala yanapimwa kimkakati ili kuwezesha wawekezaji kufanya shughuli zao kwa urahisi. Miongoni mwa matumizi yaliyopangwa katika maeneo yaliyo karibu na bandari ya Kwala ikiwemo Kibaha na Chalinze ni Makazi, Viwanda pamoja na maeneo ya biashara.

Lengo la mradi wa bandari kavu ya Kwala ni kupunguza mrundikano wa mizigo katika bandari ya Dar es Salaam na kukuza uchumi kupitia usafirishaji wa bidhaa kuelekea mikoa mingine na nchi jirani. Eneo la bandari kavu ya Kwala litakapokamilika litakuwa na miundombinu ya reli, barabara, umeme, maji na huduma za kijamii zitakazorahisisha shughuli za uendeshaji katika bandari hiyo na eneo la mradi kwa ujumla.

# TRC YASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI MEI MOSI

**Na Mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania – TRC limeungana na wafanyakazi nchini kuadhimisha sikukuu ya wafanyakazi Duniani Mei Mosi ambapo kauli mbiu kwa mwaka 2022 ni "Mishahara na maslahi bora wafanyakazi ndiyo kilio chetu, kazi iendelee" sherehe hizo zimefanyika kitaifa jijini Dodoma katika uwanja wa Jamhuri, Mei 01, 2022.

Lengo la maadhimisho ya sikukuu ya wafanyakazi ni kuwakutanisha wafanyakazi wote nchini kwa kutambua na kuenzi mchango wao mkubwa katika ujenzi wa Taifa.




Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania wakiwa wamebeba mabango yenye jumbe tofauti wakati wa sherehe ya maadhimisho ya siku ya wafanyakazi Duniani iliyofanyika Dodoma Mei 1, 2022.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan aliyekuwa mgeni rasmi amewahakikishia wafanyakazi wote kuwa Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea kuboresha maslahi ya wafanyakazi na kuboresha mazingira ya kazi ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Rais amesema hayo tarehe 01 Mei, 2022 katika sherehe za maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani zilizofanyika kitaifa katika uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma na kuhudhuriwa na viongozi wakuu wakiwemo Makamu wa Rais Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Spika wa Bunge Dkt. Tulia Ackson, Katibu Mkuu Kiongozi, Mawaziri, wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama na wafanyakazi wakiongozwa na Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzani (TUCTA).

Rais Samia Suluhu Hassan amewahakikishia wafanyakazi kuwa ahadi ya kuwaongezea Mshahara aliyoitoa mwaka jana wakati wa sherehe za Mei Mosi jijini Mwanza ipo pale pale na liko katika utekelezaji. Akihutubia wakati wa sherehe za mwaka huu za siku ya wafanyakazi Duniani zinazofanyika Mkoani Dodoma, Rais Samia amesema "lile jambo letu lipo ila sio kama lilivyosemwa na TUCTA" akimaanisha utekelezaji wa ahadi hiyo upo pale pale.

"Ninakubaliana nanyi kwamba viwango vya mishahara vya sasa havikidhi mahitaji, ili kuendelea kulinda maslahi ya Wafanyakazi, Serikali imeshaunda Bodi za Kima cha Chini cha Mishahara kwa sekta zote na tayari zimeanza kufanya tathmini ili kufanya maboresho."- Rais Samia Suluhu Hassan alisema.

Inaendelea Uk. 5

# TRC YASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA WAFANYAKAZI DUNIANI MEI MOSI



Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya maadhimisho ya siku ya wafanyakazi duniani iliyofanyika Dodoma Mei 1, 2022.

**Inatoka uk. 4**

Sambamba na Ushiriki wa TRC katika maadhimisho hayo kitaifa, Mhe. Rais ametoa zawadi kwa wafanyakazi bora 27 kwa mwaka 2022, ambapo miongoni mwa wafanyakazi bora hao kitaifa Bw. Emmanuel Siwingwa kutoka TRC amezawadiwa pesa taslimu milioni 3, hata hivyo Mhe. Rais amekabidhi makombe mbalimbli kwa wanamichezo huku wizara ya uchukuzi ikiibuka kidedea kwa kubeba makombe 7 huku timu wizara ya uchukuzi ikiibuka mshindi wa jumla wa mashindano ya michezo ya Mei Mosi mwaka 2022.

Mara baada ya maadhimisho kuhitimishwa na Mhe Rais, Kaimu Mkurugenzi i wa Shirika la Reli Tanzania Bi. Amina Lumuli alianda hafla fupi ya kuwapongeza wafanyakazi wa TRC ambapo alianza kwa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba ambayo imepeleka ujumbe moja kwa moja kwa wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania na kuwataka wafanyakazi wote kufanyakazi na kutimiza wajibu kwa maslahi mapana ya Shirika na maendeleo ya Taifa.

Vile vile, Kaimu Mkurugenzi amekabidhi Hundi kama zawadi kwa Wafanyakazi Bora na Hodari wa Shirika kwa mwaka 2022, wafanyakazi bora hao ni kutoka Makao Makuu, Kanda ya Dar es Salaam, Tanga na Tabora. Bw. Paulinus Mbehoma kutoka Idara ya Rasilimali Watu na Utawala amepewa zawadi ya milioni 2 akiwa ni mfanyakazi hodari wa Shirika kwa mwaka 2022.

Hata hivyo, Kaimu Mkurugenzi amewapa zawadi wafanyakazi hodari wengine kama Bw. Isiaka Khalid na Bw. Charles Lukindo kutoka kanda ya Tanga, Bi. Tutu Mugwe na Bw. Kagoma Malegesi kutoka kanda ya Dar es Salaam, Bw. Salum Shomali na Bw. Leth Sanga kutoka kanda ya Tabora.

Kaimu Mkurugenzi alimaliza kwa kuwashukuru wafanyakazi wote na kuwaomba zawadi hizo ziwe motisha kwa wafanyakazi wengine waweze kuchapa kazi zaidi na hatimaye kutimiza malengo ya Shirika.

# TRC YALIPA FIDIA WALIOPISHA NJIA YA UMEME SGR DODOMA NA SINGIDA



Afisa masuala ya kijamii TRC Bi. Tumaini Rikanga akizungumza na wananchi wa kijiji cha Mzogole waliotwaliwa maeneo yao kupisha ujenzi wa miundombinu ya umeme wa reli ya kisasa - SGR Morogoro - Makutupora kabla ya zoezi la fidia kuanza wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, Mei 2022

**Na mwandishi wetu**

Shirika la Reli Tanzania limefanya malipo ya fidia katika kipande cha pili cha mradi wa reli ya Kisasa SGR Morogoro - Makutopora katika wilaya ya Bahi mkoa wa Dodoma na Manyoni mkoani Singida mwezi Mei 2022.

Malipo hayo yamefanyika kwa wananchi waliotwaliwa maeneo yao kwaajili ya kupisha eneo la ujenzi wa njia ya umeme wa SGR katika kipande cha Morogoro - Makutupora.

Fidia zimelipwa kwa wanakijiji wa vijiji vya Nagulo, Mzogole na Kigwe wilaya ya Bahi mkoani Dodoma, vilevile katika kijiji cha Lusilile wilaya ya Manyoni - Singida na wakazi wote waliolipwa fidia wamepisha njia ya umeme.

Mthamini Ardhi Halmashauri ya Bahi Bi. Nuru Salei amesema wananchi walipewa elimu kabla ya maeneo yao kutwaliwa na vilevile walipatiwa elimu ya uthaminishaji ardhi na kufikia mariadhiano ya kuachia maeneo ili kupisha miundombinu ya umeme katika maeneo hayo.

Mwenyekiti wa kijiji cha Mzogole Bwana John Nzala amewapongeza wananchi wake kwa kuonesha utulivu kuanzia uthamini wa ardhi hadi kufikia malipo.

"Vilevile naishukuru TRC na Serikali kwa kupitisha reli ya SGR kijijini kwetu kwani itatusaidia kwa shughuli za kiuchumi ikiwemo kusafirisha bidhaa za biashara kwa wakati pamoja na kuturahisisishia usafiri kwenda Dar es salaam na Morogoro" John Nzala alisema.

Mpimaji Ardhi kutoka Shirika la Umeme Nchini - TANESCO kanda ya kati Alphonce Mwandu amepongeza zoezi la ulipaji fidia pia amewapongeza wananchi kwa kuweza kutoa maeneo yao kupisha ujenzi wa miundombinu ya umeme kwaajili ya kufanikisha mradi wa reli ya Kisasa mkoani Dodoma uendelee.

# SGR KUWA CHACHU YA MAENDELEO VIJIJINI

Shirika la Reli Tanzania - TRC linaendelea na zoezi la kutwaa ardhi katika maeneo mbalimbali kupisha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha tano Isaka - Mwanza wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza Mei, 2022.

Vijiji vilivyopitiwa na mradi wa SGR katika wilaya hiyo ni pamoja na Nkalalo, Ligembe na kijiji cha Isunga ambapo maeneo kadhaa ya makaburi ya wapendwa wao yamehamishwa ikiwemo eneo litakalopita njia kuu ya reli ya SGR pamoja sehemu za kuchukua vifusi.

Afisa masuala ya kijamii kutoka TRC Bi. Joyce Ponela ameeleza kuwa wananchi wanapata fursa ya kupewa kazi za zoezi katika maeneo yao ili kuweza kujipatia kipato na pia kuendelea kunufaika na mradi.

“Tunatoa kipaumbele cha kuchukua vibarua katika eneo husika ili kumpa fursa kila mwananchi kujipatia kipato” alisema Bi. Joyce.

Aidha, Bi. Joyce alisema kuwa zoezi hilo linazingatia taratibu za kiafya pamoja na haki zote za kijamii pamoja na kuruhusu wananchi kufanya mila zao na maombi kabla ya zoezi kufanyika.

“Tuna imani tofauti hasa vijijini mambo ya mila bado yanaendelea hivyo tunawapatia nafasi wananchi kufanya mila zao” alisema Bi. Joyce.

Naye Afisa Tarafa katika tarafa ya Ibindo wilayani Kwimba Bw. James Chuwa alisema kuwa wananchi wanaendelea kupata uelewa wa kuwa na eneo maalumu la maziko katika vijiji ili kuweka mpangilio mzuri wa ardhi na makazi katika maeneo yao.

“Tunajitahidi kutoa elimu hasa katika mazoezi kama haya ili kuwafumbua macho wanakijiji waache mambo ya kizamani na kufuata nyakati kadri zinavyobadilika ili kuleta maendeleo katika maeneo yao” alisema Bw. Chuwa.

Mwananchi kutoka kijiji cha Ligembe Bw. Baraka Kiberiti ameipongeza Serikali ya awamu ya sita kwa kuendeleza ujenzi wa reli ya kisasa pamoja na kutoa fursa za kazi kwa vijana katika maeneo yao na kuzidi kuhamasisha maendeleo vijijini.

“Mimi kama kijana nafurahi sana kupata fursa ya kufanya kazi katika mradi wa SGR, vijana ndio nguvukazi ya nchi yetu tukazane kufanya kazi kwa juhudi” alisema Bw. Kiberiti.

Zoezi hilo la kutwaa ardhi kupisha mradi wa SGR kipande cha tano Isaka - Mwanza ni zoezi endelevu ambapo hadi sasa hatua ya ujenzi katika kipande hicho kimefikia zaidi ya asilimia 6.



Afisa Tarafa kutoka Tarafa ya Ibindo Bwana James Chuwa akiwafahamisha wananchi wa kijiji cha Nkalalo kuhusu taratibu za zoezi la kuhamisha makaburi lililofanyika kijiji cha Nkalalo wilaya ya Kwimba hivi karibuni Mei, 2022.

# MAENDELEO YA MRADI WA RELI YA KISASA MWANZA - ISAKA SASA NI 6%



Muonekano wa kambi ya mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa Mwanza - Isaka iliyopo Malampaka mkoani Simiyu.



Sehemu ya tuta la reli ya kisasa ambalo linaendelea kujazwa udongo kabla ya kuweka reli katika kipande cha mradi wa SGR Mwanza - Isaka.



Muonekano wa kiwanda cha kuzalisha mataruma ya reli ya kisasa ikiendelea Seke wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga.ambacho ujenzi wake unaendelea.



Mtambo wa kuzalisha kokoto kwaajili ya ujenzi wa reli ya kisasa Mwanza - Isaka uliopo Seke mkoani Shinyanga.



Moja kati ya vivuko vya wanyama katika mradi wa reli ya kisasa Mwanza - Isaka kikiwa kimekamilika.



Kazi ya ujenzi ikiendelea katika moja kati ya vivuko vya wanyama katika mradi wa reli ya kisasa Mwanza - Isaka.

# TRC YASHIRIKI KAMPENI YA UTOAJI CHANJO YA POLIO WAKATI WA SAFARI



Mganga Mkuu wa Zahanati ya Shirika la Reli Tanzania Dkt. Peter Mathew akitoa elimu ya chanjo ya Polio kwa wazazi katika stesheni ya Kamata jijini Dar es Salaam Mei, 2022

Shirika la Reli Tanzania - TRC kupitia Zahanati ya Reli jDar es Salaam limetoa chanjo ya Poli kwa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano katika stesheni ya Kamata jijini Dar es Salaam kuanzia Mei 2022.

Miongoni mwa waliopata fursa ya chanjo ni abiria pamoja na wananchi wanaoishi karibu na stesheni ya Kamata ambao waliweza kufika na kupata chanjo bure

Akieleza hali ya utoaji chanjo Mganga Mkuu wa Zahanati ya Shirika la Reli Bw. Peter Mathew amesema kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya imeanzisha kampeni ya chanjo kwa watoto walio chini ya miaka mitano dhidi ya ugonjwa wa Polio ikiwa ni tahadhari ya kujikinga na ugonjwa wa Polio.

Dkt. Peter ameongeza kuwa TRC ni mdau mkubwa wa usafirishaji, hivyo Shirika limeamua kutoa chanjo ndani ya treni kuanzia stesheni ya Dar es Salaam kuelekea Morogoro, Dodoma, Tabora, Kigoma, Mwanza, Mpanda, Moshi na Arusha.

Aidha, Mganga Mkuu alitoa tathimini kuwa zoezi la utoaji chanjo litadumu kwa muda wa siku 3 ambapo limefanyika Mei 19 hadi Mei 21, 2022 huku lengo la zahanati ya Shirika ni kuchanja watoto 600.

Mganga Mkuu ameongeza kuwa huduma ya utoaji chanjo inatolewa kwenye stesheni, zahanati ya reli na kwenye treni za abiria za bara na mjini wakati wa safari ili kuhakikisha watoto wote wanao safiri wanapata chanjo.

“Zoezi linaendelea vizuri na mwitikio ni mkubwa kutokana na uhamasishaji uliofanyika kwa kina na kufanya wananchi na abiria kuitikia vizuri ingawa wachache sana wamekuwa wagumu. Niendelee kuwaomba abiria na wananchi wote wanaotumia usafiri wa treni wasiwe na wasiwasi kwani huduma hii ni endelevu na tunatoa muda wote abiria awapo safarini ” amesema Mganga Mkuu.

Kwa upande wake Bi. Angel Temba mmoja wa abiria anayesafiri kutoka Dar es Salaam mpaka Moshi ameipongeza Serikali na Shirika la reli Tanzania kwa kuwaletea huduma ya chanjo karibu wakati wa safari na kuwafanya wazazi kusafiri huku wakiwa na uhakika wa afya za watoto wao sambamba na kutekeleza adhima ya Wizara ya Afya ya kuwataka watoto wote wapate chanjo ya Polio.



**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**
**Barabara ya Sokoine**
**S.L.P 76959**
**Dar es Salaam**
**TANZANIA**
**Barua pepe; info@trc.co.tz**
**Simu ya Bure; 0800 110 042**

**Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano**
**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

| | |
|---|---|
| **MHARIRI MKUU** | **Jamila Mbarouk** |
| **MHARIRI MSAIDIZI** | **Sami Omary** |
| **MAKALA** | **Aziza Charles & Hemed Mohamed** |
| **HABARI** | **Amina Juma**<br>**Mariam Katunge** |
| **PICHA** | **Seleman Kadiko**<br>**Hassan Said** |